

i. الإظهار Al-Idhwaar - Kudhihirisha

Maana yake ni kukibainisha kitu wazi.

Katika hukmu za Tajwiyd ni kuitoa kila herufi katika makhraj yake bila ya kuweko na ghunnah. Nayo hutokea pale Nuwn saakinah au tanwiyn inapofuatiwa na mojawapo wa herufi sita za al-halq (koo)

ء ه ح خ ع غ

zinazopatikana katika ibarah ifuatayo:

أخي هاك علماً حازه غير خاسر

Mifano Ya الإظهار Al-Idhwaar<sup>1</sup>

Nuwn saakinah ن		
Idhwaaru nuwni saakinah katika maneno mawili	Idhwaaru nuwni saakinah katika neno moja	Herufi
فَمَنْ أَسْلَمَ	وَيَسْتَوُونَ	ء
مِنْ هَادٍ	وَأَنْهَرًا	ه
مِنْ عَمَلِهِمْ	أَنْعَمْتَ	ع
فَمَنْ حَاجَّكَ	وَأَنْخَرًا	ح

<sup>1</sup> Katika misahafu, nuwn saakinah inapokuwa katika hukmu hii ya الإظهار (idhwaar) aghlabu huwa imetiwa alama ya sukuwn. Ama nuwn ya idghaam na ikhfaa huwa haitiwi sukuwn.

مِنْ غَلِيٍّ	فَسَيُغْضُونَ	غ
مِنْ خَيْرٍ	وَالْمُنْخَنِقَةُ	خ

Tanwiyn			
Idhwhaaruu tanwiynu katika maneno mawili (dhwammataan)	Idhwhaaruu tanwiyni katika maneno mawili (kasrataaan)	Idhwhaaruu tanwiyn katika maneno mawili (fat-hataan)	herufi
رَسُولٌ أَمِينٌ	عَيْنٌ ءَانِيَةٌ	كُفُوا أَحَدًا	ء
سَلَامٌ هِيَ	قَوْمٌ هَادٍ	فَرِيقًا هَدَى	ه
سَمِيعٌ عَلِيمٌ	خُلُقٌ عَظِيمٌ	شَاكِرًا عَلِيمًا	ع
عَزِيزٌ حَكِيمٌ	مُلْتَقٍ حِسَابِيَّةٍ	تَجْرَةً حَاضِرَةً	ح
عَزِيزٌ غَفُورٌ	مَاءٌ غَيْرٌ	قَوْمًا غَضِبَ	غ
كَرَّةٌ خَاسِرَةٌ	شَيْءٌ خَلَقَهُ	أَزْوَاجًا خَيْرًا	خ